# JARIDA LA

# CHUO KIKUU CHA SAYANSI NA TEKNOLOJIA MBEYA (MUST)

Toleo No. 04 | Januari 2026 | MUST







# SALAMU YA MAKAMU MKUU WA CHUO

### *Prof. Aloys Ntanturo Mvuma*



Ndugu msomaji na mdau wetu, karibu katika toleo la 4 January 2026 la jarida la Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST). Kupitia Jarida hili, utapata fursa ya kusoma taarifa na kupata matukio mbalimbali kuhusu maendeleo ya Chuo kwa ujumla. Nitumie fursa hii kukutaarifu kwamba, katika mwaka wa fedha 2025/26, Chuo kimeendelea kupiga hatua kubwa za maendeleo hususani katika kupanua miundombinu ya kitaaluma kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET). Huu ni mradi wa kimkakati unaolenga katika kuimarisha uwezo wa Chuo wa kuongeza udahili wa wanafunzi na kutoa elimu bora inayokidhi mahitaji ya soko la ajira. Kwa ujumla, mradi huu una thamani ya Dola za Kimarekani milioni 31.5 ambazo ni takribani Shilingi bilioni 73 za Kitanzania.

Sambamba na utekelezaji wa vipaumbele vingine vya mradi, mradi huu umehusisha ujenzi wa jumla ya majengo matano (5) yenye thamani ya Shilingi bilioni 44.63. Kati ya majengo hayo, majengo matatu (3) yamejengwa katika kampasi kuu iliyopo katika Mkoa wa Mbeya na majengo mawili (2) yamejengwa katika Kampasi ya Mkoa wa Rukwa. Majengo yalioyopo katika kampasi ya Mbeya ni pamoja na Jengo la Taaluma lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 3,340, Karakana (wanafunzi 650) na Kituo cha Ubunifu na Uhaulishaji wa Teknolojia (wanafunzi 705).

Aidha, kwa upande wa Kampasi ya Rukwa, ujenzi wa miundombinu mipya unahusisha Jengo la Taaluma lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,920 pamoja na Karakana zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 550 kwa wakati mmoja. Ujenzi umekamilika kwa asilimia 100 na majengo yote yanaendelea kutumika kwa shughuli za kitaaluma. Kukamilika kwa ujenzi wa majengo haya kunaifanya MUST kuwa Taasisi ya kwanza nchini kati ya Taasisi zote zinazonufaika na mradi wa HEET, kukamilisha ujenzi wa majengo yote ya mradi wa wakati.

Sambamba na mafanikio haya, ninapenda nichukue fursa hii pia niwataarifu wadau wote kwamba, Chuo kimefanikiwa kuanzisha Kampasi mpya iliyopo katika Mkoa wa Mtwara. Kampasi hii imeanzishwa kwa kurithi miundombinu ya vyuo viwili vilivyofahamika kama Chuo cha Ualimu Mtwara Kawaida na Chuo cha Mtwara Ufundi. Kampasi hii ambayo kwa sasa inafahamika kwa jina la Kampasi ya Mtwara ya Ualimu wa Ufundi ni mahususi kwa ajili ya ya kutoa mafunzo ya ualimu wa amali za ufundi. Uanzishwaji wa Kampasi hii unaenda sambamba na utekelezaji wa sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Toleo la 2023 inayosisitiza mafunzo ya amali katika ngazi zote za elimu. Napenda kutumia fursa hii kuwakaribisha wazazi, walezi, wanafunzi na wadau wote katika kamapasi mpya ya Mtwara. Kampasi hii ina miundombinu inayojitosheleza kwa ajili ya kutolea mafunzo ikiwa ni pamoja na nafasi za kutosha za hosteli kwa ajili ya huduma za malazi kwa wanafunzi.

Ndugu msomaji na mdau wa MUST, jarida hili linaangazia taarifa na matukio mbalimbali muhimu ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya. Ni matarajio yangu kwamba utaendelea kujielimisha kuhusu masuala mbalimbali ya Chuo kupitia jarida hili na matoleo mengine yanayofuata.

*Nakutakia usomaji mwema.*

**Prof. Aloys N. Mvuma**
**Makamu Mkuu wa Chuo**



# UJUMBE WA MHARIRI MKUU

## Prof. Said Ali Vuai

**Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma**

Ni furaha kubwa kukukaribisha katika toleo namba 4 la Jarida la Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), linaloangazia matukio muhimu, mafanikio na hatua za maendeleo ambazo chuo kimeendelea kuzifikia katika kipindi cha hivi karibuni. Toleo hili linabeba habari zinazoonesha dhamira ya MUST katika kuimarisha ubora wa elimu ya juu, utafiti, ubunifu na ushirikiano wa kitaifa na kimataifa.

Miongoni mwa habari kuu katika toleo hili ni mafanikio ya Kongani la kitaaluma na Mkutano Mkuu wa mwaka 2025, pamoja na Mahafali ya 13 ya MUST, matukio yanayoonesha mchango wa chuo katika kuzalisha wataalamu wenye ujuzi na weledi kwa maendeleo ya taifa. Aidha, tunakuletea taarifa kuhusu Wiki ya Utafiti na Ubunifu 2025, jukwaa muhimu linalokuza ubunifu, utafiti na fursa za ajira.

Toleo hili pia linaangazia hatua za kuimarisha miundombinu ya chuo kupitia mradi wa HEET, kukabidhiwa kwa Kampasi ya Mtwara kwa wakandarasi, pamoja na maboresho mengine yanayolenga kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Pia tunaripoti kuhusu kuimarika kwa ushirikiano wa kimataifa kupitia makubaliano kati ya MUST na Samara State Technical University ya Urusi, pamoja na juhudi za kukuza ujuzi wa kidijitali kwa kushirikiana na UNIHUBS.

Habari nyingine katika toleo hili zinahusu Mhadhara wa 7 wa Umma, mafunzo ya uongozi kwa viongozi wa MUSTSO, ushiriki wa MUST katika mashindano ya SHIMMUTA Morogoro, pamoja na wanagenzi 310 waliohitimu mafunzo ya kozi mbalimbali chuoni.

Kwa ujumla, matukio haya yanaakisi safari ya MUST ya kuendelea kukua na kuimarika kama taasisi inayoongoza katika elimu ya sayansi, teknolojia na ubunifu. Tunawashukuru wadau wote wa chuo kwa mchango wao katika kufanikisha hatua hizi.

*Karibu...*

**Prof. Said A. Vuai**

**Mhariri**
**MUST Newsletter**

# YALIYOMO


| | | |
|---|---|---|
| 01 | MUST Yaonesha Ukuaji Mkubwa Katika Kongano la Kitaaluma na Mkutano Mkuu wa Mwaka 2025 | 4 |
| 02 | Mahafali ya 13 ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha MUST – 2025 | 5 |
| 03 | MUST Yaandaa Wiki ya Utafiti na Ubunifu 2025 Kuboresha Ajira na Maendeleo Endelevu | 6 |
| 04 | Kampasi ya Mtwara yakabidhiwa kwa wakandarasi, masomo kuanza rasmi 2025/2026 | 7 |
| 05 | Makamu Mkuu wa Chuo Akutana na Watumishi wa MUST Kujadili Mafanikio, Changamoto na Mwelekeo wa Baadaye | 8 |
| 06 | MUST yakabidhiwa majengo mapya ya mradi wa HEET – kampasi kuu na rukwa kampasi | 9 |
| 07 | MUST Yasaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano na Samara State Technical University ya Urusi | 10 |
| 08 | Uongozi wa MUSTSO wapatiwa mafunzo elekezi ya uongozi na utawala bora | 11 |
| 09 | MUST Yaandaa Mhadhara wa 7 wa Umma wa Mwaka 2025 Kuhusu Umekanizishaji wa Kilimo cha Wakulima Wadogo | 12 |
| 10 | MUST yashiriki katika mashindano ya SHIMMUTA Morogoro | 14 |
| 11 | Miundombinu ya kisasa ya mradi wa HEET kuanza kutumika | 15 |
| 12 | TCU yaridhishwa na miundombinu ya MUST, yaahidi makubwa | 17 |
| 13 | MUST kwa ushirikiano na UNIHUBS Yaweka Msingi wa Ujuzi wa Kidijitali | 19 |
| 14 | Makamu Mkuu wa Chuo Awahimiza Wanafunzi Wapya Nidhamu, Ubunifu na Uwajibikaji | 20 |
| 15 | Wanagenzi 310 wahitimu mafunzo ya kozi mbalimbali Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) | 21 |

# 01 MUST Yaonesha Ukuaji Mkubwa Katika Kongano la Kitaaluma na Mkutano Mkuu wa Mwaka 2025

Mbeya — Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) kimeendelea kuandika historia ya maendeleo baada ya kuadhimisha kwa mafanikio Kongano la Kitaaluma la mwaka 2025 sambamba na Mkutano Mkuu wa 11 wa Mwaka. Tukio hilo lililowakutanisha wahitimu, wafanyakazi, wanafunzi na wageni waalikwa lilitumika kama jukwaa la kutathmini mafanikio ya chuo katika nyanja za taaluma, miundombinu, na ubunifu..

Akifungua Mkutano Mkuu wa Kongona la Kitaaluma, Rais wa Kongano , Prof. Joseph Msambichaka, aliwapongeza wanachama kwa ushiriki wao endelevu katika shughuli za Kongano na kuhimiza kuongezwa kwa idadi ya wanachama pamoja na kuimarishwa kwa mchango wa wahitimu katika maendeleo ya chuo. Alibainisha mafanikio yaliyopatikana kwa mwaka mmoja uliopita ikiwemo uzalishaji wa vipeperushi, jarida la Kongano la Kitaaluma na kuongezeka kwa ushiriki wa wahitimu katika shughuli mbalimbali za chuo.

Kwa upande wake, Katibu wa Kongano la Kitaaluma, Prof. Said Ali Vuai, aliwahimiza wahitimu wa MUST kulipa ada za uanachama na kujisajili katika mfumo wa wahitimu (alumni portal), akisisitiza kuwa jumuiya imara ya wahitimu ni nguzo muhimu katika kufanikisha malengo ya maendeleo ya chuo na kuimarisha ushirikiano na wadau.

Katika hotuba yake wakati wa ufunguzi rasmi wa sherehe za Kongano, Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Aloys Mvuma, alieleza hatua kubwa zilizopigwa na MUST katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita. Alitaja ujenzi wa mabweni mawili mapya yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 800, pamoja na ujenzi wa majengo mawili ya warsha yaliyojengwa na kukamilishwa chini ya Mradi wa HEET. Aliongeza kuwa chuo kimeimarisha uwezo wake wa kitaaluma kwa kuwa na wahadhiri 58 wenye Shahada za Uzamivu na 44 wenye Shahada za Uzamili.

Prof. Mvuma pia alieleza maboresho ya kitaaluma yaliyofanyika ikiwemo marekebisho ya mitaala yote 10, ununuzi wa vitabu vipya kwa ajili ya maktaba ya chuo, pamoja na kuanzishwa kwa studio za kidijitali na madarasa janja kwa ajili ya kuboresha mbinu za kisasa za ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, alitaja kuimarishwa kwa shughuli za Kituo cha Ubunifu na Uhawilishaji Teknolojia na kuanzishwa kwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya Kampasi ya Mtwara kama hatua muhimu ya upanuzi wa MUST.



| Wajumbe wa kongano la kitaaluma wakifuatilia mwenendo wa Mkutano -Ukumbi wa Nyerere MBEYA

Mgeni rasmi katika tukio hilo, Bw. Jumanne Mtambalike, mjasiriamali na mwanzilishi mwenza wa Sahara Ventures, alitoa muhadhara kuhusu nafasi ya Afrika katika enzi ya mashine na ustaarabu wa kidijitali. Aliwahimiza wanafunzi na wahitimu kujifunza na kutumia maarifa ya akili bandia (AI), akisisitiza kuwa watakaotumia AI kwa ufanisi ndio watakaokuwa na ushindani mkubwa katika soko la ajira.

Sherehe hizo zilihitimishwa kwa utoaji wa tuzo kwa wanafunzi waliofanya vizuri kitaaluma mwaka 2025. Bw. Joshua Write Martin, mwanafunzi wa Shahada ya Sayansi ya Chakula na Teknolojia, alitangazwa mwanafunzi bora wa kiume kwa kupata GPA ya 4.9 kati ya 5.0, huku tuzo ya mwanafunzi bora wa kike ikitolewa kwa Bi. Fausta Peter Mroto, mwanafunzi wa Stashahada ya Sayansi ya Chakula na Teknolojia, aliyepata GPA ya 4.8 kati ya 5.0.

Kwa ujumla, kongamano la kitaaluma ya Convocation na Mkutano Mkuu wa Mwaka 2025 yameonesha mwelekeo chanya wa MUST katika safari yake ya mageuzi, yakidhihirisha dhamira ya uongozi, wafanyakazi, wahitimu na wadau wa chuo katika kujenga taasisi bunifu, inayokidhi mahitaji ya kizazi cha kidijitali na kuchangia maendeleo endelevu ya taifa.



*Walioketi, Prof. Aloyce N. Mvuma (katikati), Makamu Mkuu wa Chuo na Mgeni Rasmi wa Kongano la kitaaluma akiwa kwenye picha ya pamoja na viongozi mbalimbali*

# 02 MAHAFALI YA 13 YA CHUO KIKUU CHA SAYANSI NA TEKNOLOJIA MBEYA(MUST) – 2025

Mahafali ya 13 ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya (MUST) yalifanyika kwa mafanikio makubwa tarehe 5 Desemba 2025 katika viwanja vya Maktaba ya Magufuli, yakiongozwa na Mkuu wa Chuo, Dkt. Amani Abeid Karume. Hafla hiyo pia ilihudhuriwa na Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Aloys Mvuma, pamoja na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Mhe. Zakia Hamdan Meghji.

Sherehe zilianza kwa salamu za Mlawi wa Chuo, Dkt. Hadija Matimbwa, ambaye aliwakumbusha wahitimu umuhimu wa kuwa mabalozi wema wa MUST ndani na nje ya Tanzania. Baada ya hotuba yake, Dkt. Matimbwa alimkaribisha Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Aloys Mvuma, ambaye aliwatambulisha wageni mbalimbali waalikwa waliofika kushuhudia mahafali hayo ya kihistoria.



*Mhe. Dkt. Aman Abeid Karume, (katikati) Mkuu wa Chuo na Rais wa zamani wa serikari ya mapinduzi ya zanzibar, Mhe. Zakia medj hamdan (kulia) Mwenyekiti wabaraza la Chuo, Prof. Aloyce N. Mvuma (kushoto), Makamu Mkuu wa Chuo kwenye picha ya pamoja na viongozi mbalimbali*

Kabla ya kuanza rasmi kwa zoezi la kutunuku, Mkuu wa Chuo, Dkt. Karume, alitembelea na kukagua maonyesho ya bunifu na teknolojia mbalimbali zilizobuniwa na wanafunzi wa MUST, akipongeza ubunifu na ari ya wanafunzi katika kutatua changamoto za jamii.

Katika mahafali hayo, Dkt. Karume alitunuku Astashahada, Stashahada, Shahada, Shahada za Umahili na Shahada za Uzamivu kwa jumla ya wahitimu 2,875. Kati yao, 766



*Mhe. Dkt. Aman Abeid Karume, Mkuu wa Chuo akitunuku Shahadi mbalimbali kwa wahitimu wa Mhafari ya 13*
***-MUST Mbeya***

walikuwa wanawake na 2,109 wanaume, idadi inayoonyesha maendeleo katika usawa wa kijinsia na ongezeko la wataalamu wapya katika sekta mbalimbali.

Baada ya kutunuku wahitimu, Mkuu wa Chuo alitembelea majengo ya Mradi wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET), mradi ambao umekabidhiwa hivi karibuni na unaotarajiwa kuongeza uwezo wa chuo katika kutoa mafunzo ya kisasa na kukuza tafiti zenye tija.

Mahafali ya mwaka 2025 yameacha alama muhimu katika historia ya MUST, yakidhihirisha dhamira ya chuo kuendelea kutoa elimu bora, kuendeleza ubunifu, na kutengeneza wataalamu wenye mchango mkubwa kwa maendeleo ya taifa.



*Wahitimu wa Mahafari ya 13 wakiwam kwenye picha ya pamoja*

# 03 MUST Yaandaa Wiki ya Utafiti na Ubunifu 2025 Kuboresha Ajira na Maendeleo Endelevu

Mbeya — Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) kimefanikiwa kuandaa Wiki ya Utafiti na Ubunifu (Research and Innovation Week – RIW) ya mwaka 2025, tukio lililowakutanisha wanafunzi, watafiti, wabunifu na wataalamu kutoka sekta binafsi chini ya kaulimbiu

> *Kukusanya Mafunzo, Utafiti, Ubunifu na Sekta kwa Mustakabali Endelevu na Jumuishi.*

Akifungua rasmi wiki hiyo, Prof. Aloys Mvuma alisisitiza umuhimu wa utafiti na ubunifu katika kutatua changamoto za jamii. Alihimiza wanafunzi na watafiti kuandaa ubunifu unaolenga kutatua matatizo halisi yanayokabili jamii, akibainisha kuwa utafiti unaofanywa kwa ufanisi hubadilisha changamoto kuwa fursa. Alibainisha pia nafasi ya Kituo cha Ubunifu na Uhawilishaji Teknolojia (CITT), hasa sasa baada ya kukamilika kwa miundombinu ya kisasa chini ya Mradi wa HEET, ikitoa fursa kwa wanafunzi na wabunifu wadogo kuendeleza suluhisho zinazoweza kuongoza kwenye ajira binafsi na kuunda ajira kwa wengine.



*Prof. Aloys Mvuma akihutubia wakati wa ufunguzi wa wiki ya utafiti na Ubunifu iliyofanyika katika ukumbi wa Nyerere*

Baada ya ufunguzi, Dkt. Ramadhani Tekka alimtambulisha mzungumzaji mkuu wa RIW 2025, Bw. Musa K. Kamata, ambaye ni mtaalamu mashuhuri katika ubunifu na maendeleo ya teknolojia. Katika hotuba yake, Bw. Kamata alisisitiza swali muhimu: "Jinsi gani unaleta ubunifu sokoni?" Alitoa maelezo ya kina kuhusu Mfumo wa Lean Canvas, akieleza hatua kwa hatua jinsi wabunifu wanavyoweza kubadilisha mawazo kuwa bidhaa zinazokidhi mahitaji ya soko. Aliwahimiza wanafunzi kuanza kutekeleza mawazo yao ya ubunifu mapema, ili kuingia sokoni waweze kujiajiri na baadaye kuajiri wengine.



*Wabunifu walioshiriki katika ubunufu kwa mwaka 2025wakiwa katika picha ya Pamoja na menejiment ya chuo*

Mhadhara ulifuatwa na mjadala wa paneli wenye wataalamu mashuhuri: Dkt. Phesto Namayala, Dkt. Kazema, Dkt. Mulyashimbi Helikumi, na Dkt. Fredrick Ojija, ambao walijadili kaulimbiu ya tukio, wakishirikisha mitazamo mbalimbali kuhusu ubunifu, ubisharishaji na uhusiano kati ya elimu na mahitaji ya sekta. Paneli pia walijibu maswali ya washiriki, yakionyesha hamasa na shauku ya hadhira.

Miongoni mwa matukio muhimu, washiriki bora walitambuliwa kwa mchango wao. Watafiti wakiwemo Dkt. Fredrick Ojija na Dkt. Ramadhani Tekka walipata heshima ya kutambuliwa, huku wanafunzi wabunifu walioshiriki maonyesho ya miradi yao wakipokea vyeti kuthibitisha ubunifu, ari na uwezo wa kutatua changamoto.

Akihitimisha wiki hiyo, Prof. Zacharia Katambala aliwapongeza washiriki wote, akisisitiza umuhimu wa kubadilisha mawazo kuwa bidhaa zinazokubalika sokoni, na kuwahimiza wanafunzi kuchukua hatua na kutumia maarifa waliyojifunza wakati wa RIW 2025.

Wiki ya Utafiti na Ubunifu 2025 ya MUST iliisha kwa hamasa mpya na dhamira ya pamoja ya kuunda mustakabali ambapo mafunzo, utafiti, ubunifu na sekta vinashirikiana kutanua maendeleo ya jamii na kukuza maendeleo endelevu.

# 04 KAMPASI YA MTWARA YAKABIDHIWA KWA WAKANDARASI, MASOMO KUANZA RASMI 2025/2026

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (Mbeya University of Science and Technology – MUST) kimekabidhi rasmi maeneo ya ukarabati kwa wakandarasi katika Kampasi ya Mtwara, hatua inayochukuliwa kama sehemu ya maandalizi ya kupokea wanafunzi wa Shahada ya Kwanza (Bachelor Degree) kwa mwaka wa masomo wa 2025/2026.

Makabidhiano hayo yanafungua rasmi utekelezaji wa kazi za ukarabati na uboreshaji wa miundombinu ya chuo katika kampasi hiyo, hatua inayolenga kuhakikisha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji yanakidhi viwango vinavyotakiwa kwa elimu ya juu kabla ya kuanza kwa masomo ya ngazi ya shahada.

Akizungumza wakati wa zoezi la makabidhiano, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia Mipango, Fedha na Utawala, Profesa Zacharia Katambara, aliwataka wakandarasi kuhakikisha kazi zote zinafanyika kwa ubora wa hali ya juu, kwa kuzingatia taratibu, uwazi na matumizi sahihi ya rasilimali.

> *“Ni muhimu kila hatua ya utekelezaji wa mradi ihifadhiwe kumbukumbu, mawasiliano yafanyike kwa njia rasmi, na kazi itekelezwe kwa uadilifu bila ulazima wa kutoa au kupokea malipo yasiyo rasmi,” alisema* ***Profesa Katambara.***

Kwa upande wao, wakandarasi waliokabidhiwa maeneo ya kazi walieleza utayari wao wa kutekeleza majukumu waliyopewa kwa kuzingatia muda na viwango vilivyokubaliwa. Wakizungumza kwa niaba ya makandarasi, waliahidi kuwa kazi zitakamilika kwa ubora unaotarajiwa na kwa kuzingatia makubaliano ya kimkataba.



*Jengo la Utawala Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya*
***-Kampasi ya MUST Mtwara***

Makandarasi waliokabidhiwa utekelezaji wa kazi hizo ni kampuni za Kawishe Contractor, Proviamo Electrical, Gopa Contractors, Mahimbo and Company pamoja na Ventrek Enterprises. Kazi za ukarabati katika Kampasi ya Mtwara zinatarajiwa kuboresha miundombinu ya chuo na kuweka msingi imara wa kupokea wanafunzi wa shahada ya kwanza katika mwaka wa masomo wa 2025/2026.



*Walioketi, (wapili kulia) Prof. Zakaria Katambara, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo, Mipango, Fedha na Utawala kwenye picha ya pamoja na wakandarsi na Viongozi mbalimbali*
***-Kampasi ya Mtwara***

# 05 Makamu Mkuu wa Chuo Akutana na Watumishi wa MUST Kujadili Mafanikio, Changamoto na Mwelekeo wa Baadaye

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, Prof. Aloys N. Mvuma, amekutana na watumishi wote wa chuo pamoja na menejimenti ya MUST kwa lengo la kushirikishana taarifa muhimu kuhusu uendeshaji wa chuo, mafanikio yaliyopatikana, changamoto zilizopo pamoja na mipango ya maendeleo ya chuo kwa siku zijazo.

Akizungumza katika mkutano huo, Profesa Mvuma aliwapongeza wahadhiri na watumishi wa kada ya kitaaluma waliokamilisha masomo yao katika mwaka wa fedha unaoendelea, akibainisha kuwa hatua hiyo ni muhimu katika kuinua ubora wa ufundishaji, utafiti na huduma za kitaaluma ndani ya chuo.



*Prof. Aloyce N. Mvuma, Makamu Mkuu wa Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya akielezea mipango ya Taasisi wakati wa kikao na watumishi -MUST Mbeya*



*Prof. Aloyce N. Mvuma, (katikati) Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Said A. Vuai, (wapili Kushoto) Naibu Makamu Mkuu wa Chuo - Taaluma, Prof. Zakaria Katambara Naibu makamu Mkuu wa chuo Mipango, Fedha na Utawala kwenye picha ya pamoja na Miss. Mote Mahenge - Afisa Rasilimali watu na Miss. Lugando Mwakilasa - -MUST Mbeya*



*Dr. Emmanuel Mwangomo, Mwenyekiti THTU akiuliza swali kwa niaaba ya watumishi -MUST Mbeya*

Aidha, Makamu Mkuu wa Chuo aliwahimiza watumishi kutumia ipasavyo taaluma zao, maarifa waliyonayo pamoja na miundombinu ya kisasa ya chuo, hususan maabara na vifaa vya kisayansi, kama fursa ya kuzalisha mapato. Alisisitiza kuwa ni upotevu wa rasilimali endapo miundombinu yenye viwango vya kimataifa haitatumika kikamilifu kwa shughuli za kitaaluma, ubunifu na ushirikiano na wadau wa nje.

Katika hotuba yake, Profesa Mvuma alieleza pia mafanikio makubwa yaliyofikiwa na chuo katika kipindi cha hivi karibuni, yakiwemo maboresho ya mitaala ili iendane na mahitaji ya sasa ya soko la ajira, uboreshaji wa miundombinu pamoja na kuimarika kwa utoaji wa huduma kwa wanafunzi na jamii kwa ujumla. Ameongeza kuwa MUST imeendelea kuimarisha rasilimali watu kwa kuongeza idadi ya watumishi kupitia ajira mpya na uhamisho kutoka taasisi nyingine, hali iliyopelekea idadi ya watumishi kufikia 852.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala, Mote Mahenge, alihitimisha mkutano huo kwa kuwahimiza watumishi kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI. Alisisitiza umuhimu wa kuzingatia afya binafsi kwa kuishi maisha yenye mtindo bora, ikiwemo kula mlo kamili na kufanya mazoezi ya mara kwa mara ili kupunguza hatari ya magonjwa yasiyoambukiza kama kisukari na shinikizo la damu.

Kwa ujumla, mkutano huo uliendelea kuimarisha mshikamano, uwazi na ushirikiano miongoni mwa watumishi wa MUST, sambamba na kuweka mwelekeo wa pamoja katika kuendeleza chuo na kuboresha ustawi wa wafanyakazi wake.

# 06 MUST YAKABIDHIWA MAJENGO MAPYA YA MRADI WA HEET KWA PANDE MBILI

## – Makao Makuu na Rukwa Kampasi

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) kimekabidhiwa rasmi majengo mapya ya kisasa yaliyojengwa chini ya Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) kwa pande mbili — Makao Makuu na Rukwa Kampasi.

Katika hafla ya makabidhiano yaliyofanyika katika makao makuu ya chuo, Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Aloys Mvuma, alipokea Jengo la Kisasa la Taaluma kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji Mhandisi Joseph Mkisi, wa kampuni ya Malk Consultant Ltd, waliokuwa washauri elekezi wa ujenzi huo.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mhandisi Mkisi alieleza kuwa jengo hilo ni la kisasa lenye ukumbi wa mikutano unaoweza kuchukua watu 400, pamoja na maabara na madarasa yenye uwezo wa kubeba wanafunzi kati ya 40 hadi 290 kwa wakati mmoja, hivyo kuruhusu jumla ya wanafunzi takribani 3,340 kutumia jengo hilo kwa mkupuo.

Kwa upande wake, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu, Prof. Said Ali Hamad Vuai, alishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kukiwezesha chuo kupitia miradi ya maendeleo kama HEET. Alisema jengo hilo litakuwa chachu katika uratibu wa mitaala mipya 72 iliyoanzishwa hivi karibuni, kwa kuwa litatoa mazingira bora ya kujifunzia na kufundishia kwa wanafunzi na wahadhiri.

Wakati huohuo, kwa upande wa Rukwa Kampasi, MUST imekabidhiwa majengo manne, likiwemo jengo moja la kisasa la taaluma na karakana tatu kubwa zenye jumla ya vyuma zaidi ya 20, zilizojengwa na kampuni ya M/S TIL Construction Ltd.



*Prof. Aloys mvuma akishuhudia makabidhiano ya hati za ujenzi na ushauri wa kitaalam kati ya kampuni ya M/S TIL construction ltd na Chuo*

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, Meneja Mkuu wa kampuni ya M/S TIL Construction Ltd, Bw. Faraja Selemani, aliishukuru menejimenti ya chuo kwa ushirikiano mkubwa walioupata wakati wa utekelezaji wa mradi huo na kueleza kuwa majengo yote yapo tayari kwa matumizi.

Katika hotuba yake wakati wa makabidhiano hayo, Prof. Aloys Mvuma alisisitiza kwamba ujenzi wa majengo hayo utaongeza ufanisi wa masomo ya sayansi na teknolojia na kusaidia kuongeza udahili wa wanafunzi. Pia aliwasihi watumishi wa Rukwa Kampasi kutunza majengo na vifaa vyake, na kutumia fursa hiyo kuongeza vyanzo vya mapato vya chuo kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wananchi wa mkoa wa Rukwa na maeneo jirani, ili waweze kupata ujuzi utakaowawezesha kujiajiri katika fani za umeme, ujenzi na teknolojia mbalimbali.

Prof. Mvuma alihitimisha kwa kupongeza juhudi za Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, na washirika wa maendeleo wanaounga mkono utekelezaji wa mradi wa HEET, akisisitiza kuwa MUST itaendelea kutumia miundombinu hiyo mipya kuboresha ubora wa elimu na utafiti nchini.



*Picha ni jingo la taaluma lililojengwa katika makao makuu chini ya mladi wa HEET*

# 07 MUST Yasaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano na Samara State Technical University ya Urusi

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (Mbeya University of Science and Technology – MUST) kimesaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano (Memorandum of Understanding – MoU) na Samara State Technical University ya Shirikisho la Urusi, ikiwa ni hatua muhimu katika kupanua wigo wa ushirikiano wa kitaaluma na kisayansi katika ngazi ya kimataifa.

Hafla ya utiaji saini ilifanyika kwa njia ya mtandao (virtual signing ceremony) na ilishuhudiwa na ujumbe wa MUST ulioongozwa na Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Aloys N. Mvuma. Kwa upande wa Samara State Technical University, chuo hicho kiliwakilishwa na Prof. Anna Zotova, Naibu Rektor, pamoja na Aleksandra Zhelandinova, Mkuu wa Ofisi ya Mahusiano ya Kimataifa.

Akizungumza baada ya utiaji saini wa makubaliano hayo, Makamu Mkuu wa Chuo alieleza kuwa ushirikiano huo ni sehemu ya mkakati wa MUST wa kujenga mahusiano imara ya kimataifa yanayochochea ubora wa elimu, utafiti na ubunifu.

Makubaliano hayo yanalenga maeneo matano muhimu ya ushirikiano, yakiwemo kubadilishana wanafunzi na watumishi wa kitaaluma, utekelezaji wa tafiti za pamoja, ushiriki katika semina, makongamano na mikutano ya kitaaluma, kubadilishana taarifa na nyenzo za kitaaluma, pamoja na kushirikiana katika uchapishaji wa kazi za kitaaluma na kisayansi.



Prof. Anna Zotova, Makamu Mkuu wa Chuo cha cha ufundi Samara (Urusi) akionesha hati ya makubaliano

Kupitia ushirikiano huu, MUST inatarajia kuongeza fursa za mafunzo na tafiti kwa jumuiya yake ya kitaaluma, kuimarisha uwezo wa watafiti, pamoja na kuinua mchango wa chuo katika uzalishaji wa maarifa na suluhisho bunifu kwa changamoto za maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Kwa ujumla, kusainiwa kwa MoU hii kunaakisi dhamira ya pamoja ya MUST na Samara State Technical University ya kuimarisha ushirikiano wa kielimu, kukuza ubora wa elimu ya juu na kuendeleza tafiti zenye tija kwa maendeleo ya kitaifa na kimataifa.



Prof. Aloyce Mvuma, pamoja na viongozi wa chuo wakishiriki zoezi la kusaina hati ya makubaliano na Chuo cha ufundi Samara

# 08 Uongozi wa MUSTSO wapatiwa mafunzo elekezi ya uongozi na utawala bora

Uongozi wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, MUSTSO, hivi karibuni umepata mafunzo elekezi (induction training) yaliyoendeshwa na Mkurugenzi wa Huduma za Wanafunzi, kwa lengo la kuimarisha uongozi, utawala bora na uwajibikaji ndani ya jumuiya ya wanafunzi.

Mafunzo hayo yalilenga kuwawezesha viongozi wa wanafunzi kuelewa vyema majukumu yao na namna ya kuyatekeleza kwa ufanisi, kwa kuzingatia sera, kanuni na taratibu za chuo. Mada zilizofundishwa ni pamoja na masuala ya kitaaluma yanayohusu uongozi wa wanafunzi, mbinu za mawasiliano bora, ujuzi wa majadiliano (bargaining skills), pamoja na usimamizi mzuri wa muda.

Aidha, washiriki walipata mafunzo kuhusu usimamizi wa fedha, masuala ya ukaguzi (audit), namna ya kujibu hoja za ukaguzi, pamoja na misingi ya uongozi wa kimaadili. Mafunzo haya yamelenga kuwajengea viongozi wa MUSTSO uwezo wa kusimamia rasilimali za wanafunzi kwa uwazi na uadilifu, sambamba na kuimarisha uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu yao.

Kupitia mafunzo hayo, viongozi wa wanafunzi wamepata maarifa na ujuzi muhimu utakaowawezesha kuongoza kwa kuwajibika, kuwakilisha vyema maslahi ya wanafunzi, na kushirikiana kwa karibu na uongozi wa chuo katika kuboresha ustawi na mazingira ya kujifunzia.



Dr. Matungwa William, akitoa mafunzo kwa viongozi wa MUSTSO

Kwa ujumla, mafunzo haya ni hatua muhimu katika kuwaandaa viongozi wa MUSTSO kuwa viongozi bora, waadilifu na wenye maono, watakaotoa mchango chanya katika maendeleo ya wanafunzi na ustawi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya.







Viongozi mbalimbali wa Serikari ya Wanafunzi kwenye picha ya pamoja na atoa mada wakati wa mafunzo

# 09 **MUST** Yaandaa Mhadhara wa 7 wa Umma wa Mwaka 2025 Kuhusu Umekanizishaji wa Kilimo cha Wakulima Wadogo

Mbeya — Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) kimeandaa Mhadhara wa 7 wa Umma wa mwaka 2025 wenye kaulimbiu "Umekanizishaji wa Kilimo cha Wakulima Wadogo: Fursa na Changamoto Kabla na Baada ya Mavuno." Mhadhara huo uliwakutanisha wasomi, wanafunzi, wataalamu na wadau kutoka sekta ya kilimo ili kujadili changamoto zinazowakabili wakulima wadogo nchini Tanzania.

Akifungua mhadhara huo, Mgeni Rasmi ambaye pia ni Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Aloys Mvuma, alisisitiza umuhimu wa kukabiliana na upotevu wa mazao kabla na baada ya mavuno. Akirejea Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Mazao Baada ya Mavuno 2019–2029, Prof. Mvuma alisema Tanzania inapoteza kati ya asilimia 30 hadi 40 ya mazao ya nafaka, na zaidi kwa mazao yanayoharibika kwa urahisi, kutokana na uhaba wa teknolojia za uhifadhi, usimamizi na umekanizishaji wa kilimo.

Prof. Mvuma alieleza kuwa MUST, kupitia Chuo cha Sayansi na Teknolojia ya Kilimo na taasisi nyingine zilizopo ndani ya chuo, ina wajibu wa kitaifa wa kuchangia suluhisho za kisayansi na utafiti zitakazopunguza upotevu



*Dkt. Mahinda (UDSM), akitoa muhadahara kuhusu masuala ya kilimo*

wa mazao na kuongeza tija kwa wakulima. Alisisitiza kuwa uwezo wa kitaaluma na utafiti wa chuo unaweka MUST katika nafasi ya kipekee ya kuleta ubunifu unaohitajika katika sekta ya kilimo.



*Makamu wa Mkuu wa Chuo, Prof. Aloys Mvuma, akitoa hotuba ya ufunguzi wakati wa Mhadhara wa 7*

Baada ya hotuba ya ufunguzi, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Taaluma, Utafiti na Ushauri Elekezi), Prof. Asher Mwidege, alimtambulisha mzungumzaji mkuu, Dkt. Athumani Juma Mahinda kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Prof. Mwidege alieleza uzoefu mkubwa wa Dkt. Mahinda katika uhandisi wa kilimo na umekanizishaji, pamoja na mchango wake katika maendeleo ya sekta ya kilimo nchini.

Katika mhadhara wake, Dkt. Mahinda alieleza kwa kina fursa na changamoto za umekanizishaji kabla na baada ya mavuno. Alibainisha kuwa zaidi ya asilimia 85 ya uzalishaji wa kilimo nchini unatokana na wakulima wadogo, lakini wengi wao bado wanatumia zana za jadi na mbinu za kizamani. Alisisitiza kuwa matumizi ya teknolojia za kisasa yanaweza kupunguza upotevu wa mazao, kuongeza uzalishaji na kuboresha kipato cha wakulima. Aidha, alitoa wito wa kuongezwa kwa uwekezaji, mafunzo na uhawilishaji wa teknolojia ili wakulima wadogo



*Watalaamu kutoka ndaki mbalimbali wakiwa katika picha Pamoja na mtoa maada wa mhadhara Dkt .Mahinda wakati wa mjadara wa mhadhala wa 7 wa umma wa mwaka 2025*



Makamu wa Mkuu wa Chuo, Prof. Aloys Mvuma, pamoja na viongozi wengine wa chuo kwenye picha ya pamoja na mtoa mada wa muhadhara wa 7 Dkt. Mahinda



Wahadhiri na wanafunzi wakifatilia wasilisho la Dkt. Mahinda wakati wa mhadhara wa 7

waweze kumudu na kutumia zana za umekanizishaji.

Mhadhara huo uliendelea kwa mjadala wa kitaalamu uliohusisha wataalamu kutoka MUST akiwemo Dkt. Marco Mngongo na Dkt. Angela Aluko, ambao walijibu maswali kutoka kwa washiriki na kueleza tafiti zinazoendelea pamoja na teknolojia mpya zinazoweza kusaidia kuimarisha mnyororo wa thamani wa kilimo nchini.

Akihitimisha tukio hilo, Prof. Zacharia Katambara aliwapongeza wazungumzaji na washiriki kwa michango yao yenye tija. Aliwataka wasomi na watafiti, hususan kutoka vyuo vinavyohusika na umekanizishaji na uhandisi, kuongeza juhudi katika kufanya tafiti na kubuni teknolojia endelevu zitakazosaidia kupunguza upotevu wa mazao na kuboresha uzalishaji wa kilimo kwa wakulima wadogo nchini.



# 10 MUST YASHIRIKI KATIKA MASHINDANO YA SHIMMUTA MOROGORO

Shirikisho la Michezo la Mashirika ya Umma, Taasisi na Makampuni Binafsi Tanzania (SHIMMUTA) ni miongoni mwa Mashirikisho ya Michezo yaliyoanzishwa mnamo mwaka 1967 ambalo hufanya mashindano yake kila mwaka.

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) ni miongoni mwa taasisi zilizoshiriki katika mashindano ya SHIMMUTA yaliyofanyika mkoani Morogoro kuanzia tarehe 25/11/2025 hadi tarehe 6/12/2025. Katika ushiriki wake wanamichezo wa MUST walishiriki michezo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mpira wa miguu (football), mpira wa kikapo (basketball), volleyball, riadha, dats, karata na bao.



Timu ya mpira wa miguu MUST wakijiweka sawa dhidi ya SUA

Katika mashindano ya mchezo wa volleyball (wanaume), MUST ilifanya vizuri sana. Kwa ustadi na umoja wa kipekee, timu ya volleyball ya wanaume ilifanikiwa kuzishinda timu za taasisi mbalimbali walizoshindana nazo na hivyo kuingia fainali na hatimaye kushika nafasi ya pili. Wanamichezo wa volleyball wanawake wa MUST pia walijitahidi na kufanya vizuri katika michezo yao, wakionyesha kuwa timu ya wanawake pia ina nguvu na uwezo wa kushindana na timu bora za mashindano haya.

Mashindano haya ya SHIMMUTA yalitoa makombe na zawadi mbalimbali kwa washindi wa kwanza hadi wa tatu. MUST ilifanya vyema kwa kupata kombe la mshindi wa pili katika mchezo



Timu ya mpira wa wavu MUST wakiwa tayari kuwakabiri NIT

wa volleyball (wanaume) na pia ilizawadiwa jezi nzuri za volleyball kama ishara ya mafanikio yao makubwa.

Katika mashindano mengine, kama vile mpira wa miguu, mpira wa kikapu, riadha, karata, dats, na bao, wanamichezo wa MUST walijitahidi kuonyesha ufanisi wao, ingawa kulikuwa na ushindani mkali kutoka kwa taasisi nyingine. Hata hivyo, jambo muhimu zaidi lilikuwa kujivunia umoja na mshikamano waliokuwa nao, na jinsi walivyoweza kuungana kama familia moja katika mashindano haya.

Mashindano ya SHIMMUTA yaliyofanyika Morogoro yalikuwa ni jukwaa muhimu kwa taasisi mbalimbali kuonyesha vipaji vyao na kukuza ushirikiano. Mashindano haya ni muhimu sana kwa kukuza afya, uhusiano wa kijamii, na kuhamasisha mshikamano kati ya taasisi mbalimbali. Pia, kushiriki kwa MUST katika michezo mbalimbali kunasaidia kuongeza umaarufu wa taasisi na pia kuhamasisha watu wengi zaidi kushiriki michezo kwa ajili ya afya na utimamu wa mwili



Timu ya volleyball wanawake kutoka MUST wakiwa uwanjani dhidi ya TBS

11

# MIUNDOMBINU YA KISASA YA MRADI WA HEET KUANZA KUTUMIKA

Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (Mbeya University of Science and Technology – MUST) kimefanya kikao cha wadau wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya kukamilisha na kuanza matumizi ya miundombinu ya kisasa inayotekelezwa chuoni hapo. Kikao hicho ni sehemu ya jitihada za chuo katika kuimarisha ubora wa elimu ya juu na kuchochea maendeleo ya kiuchumi kupitia sayansi, teknolojia na ubunifu.

Mradi wa HEET unaotekelezwa MUST chini ya usimamizi wa Makamu Mkuu wa Chuo, Profesa Aloys N. Mvuma, unalenga kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kujenga majengo ya kisasa, kuanzisha maabara na karakana zenye vifaa vya kisasa pamoja na kuongeza ufanisi wa utoaji wa elimu inayokidhi mahitaji ya soko la ajira na maendeleo ya taifa.

Kikao hicho kiliwakutanisha wadau kutoka taasisi na vyombo mbalimbali ikiwemo Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Ofisi ya Kazi ya Mkoa, Jeshi la Polisi, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, viongozi wa serikali za mitaa, wakuu wa shule zilizo jirani na chuo pamoja na wawakilishi wa Serikali ya Wanafunzi. Ushirikishwaji wa wadau hao ulilenga kujadili masuala ya usalama, afya, mazingira ya kazi, ulinzi wa miundombinu na mahusiano kati ya chuo na jamii inayokizunguka wakati wa kuanza matumizi ya majengo na vifaa vipya.

Akifungua kikao hicho, Kaimu Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia Utawala, Mipango na Fedha, Dkt. Juma Ally, alisema mradi wa HEET utakuwa na mchango mkubwa kwa chuo, jamii na taifa kwa ujumla. Alisisitiza kuwa uwekezaji unaofanywa kupitia mradi huo utaongeza ufanisi wa ufundishaji na ujifunzaji, kuimarisha tafiti na kutoa fursa zaidi kwa wanafunzi na wahadhi-

ri katika nyanja za sayansi na teknolojia.

Baada ya majadiliano, wadau walipata fursa ya kutembelea majengo ya mradi, maabara pamoja na karakana za kisasa zilizojengwa chini ya mradi wa HEET. Katika ziara hiyo, walijionea ubora wa miundombinu na maandalizi ya matumizi ya vifaa vya kisasa, hali iliyowafanya wengi wao kueleza kuridhishwa na kazi iliyofanyika pamoja na kuthibitisha kuwa miundombinu hiyo inaendana na thamani ya fedha iliyotumika.

mkandarasi wa mradi yuko katika hatua za mwisho za maandalizi ya kukabidhi rasmi miundombinu hiyo, hatua itakayowezesha Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kuanza kutumia majengo na vifaa hivyo kikamilifu kuanzia mwanzoni mwa mwezi Novemba 2025, hatua inayotarajiwa kufungua sura mpya ya utoaji wa elimu ya juu yenye ubora na mchango chanya katika mageuzi ya kiuchumi nchini.

Baadhi ya wadau walieleza kuvutiwa na mazingira ya kisasa ya ujifunzaji yaliyopo chuoni hapo, wakisema kuwa uwekezaji huo utakuwa kichocheo cha kuimarisha elimu ya sayansi na teknolojia, kuvutia wanafunzi na wataalamu wengi zaidi na kuongeza ushindani wa chuo kitaifa na kimataifa.

Mbali na manufaa ya kitaaluma, mradi wa HEET unatarajiwa kuwa na mchango mpana kwa jamii inayozunguka chuo na uchumi wa eneo la Mbeya kwa ujumla kupitia ongezeko la ajira, shughuli za kiuchumi na ushirikiano kati ya chuo na jamii. Viongozi wa serikali za mitaa walioshiriki kikao hicho walieleza matumaini yao kuwa mradi huo utaimarisha mahusiano na kuleta manufaa ya moja kwa moja kwa wananchi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa katika kikao hicho,



*Jengo la Taaluma MUST kampasi kuu Mbeya*



*Jengo la Ubunifu na Uhauloshaji Teknolojia MUST kampasi kuu Mbeya*



*Jengo la Taaluma na Utawala MUST kampasi ya Rukwa*



*Jengo la karakana MUST kampasi ya Rukwa*




# TCU yaridhishwa na miundombinu ya MUST, yaahidi makubwa

Katibu Mtendaji wa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (Tanzania Commission for Universities – TCU), Profesa Charles Kihampa, ametembelea Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (Mbeya University of Science and Technology – MUST) kwa lengo la kujionea mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji pamoja na miundombinu inayotumiwa na wanafunzi wa chuo hicho.

Ziara hiyo ilifanyika ikiwa ni sehemu ya jukumu la TCU la kusimamia na kutathmini ubora wa elimu ya juu nchini, hususan katika kuhakikisha vyuo vina miundombinu, vifaa na mazingira yanayokidhi viwango vya kitaifa na kimataifa. Profesa Kihampa aliambatana na Mkurugenzi wa Udahili na Usimamizi wa Mifumo wa TCU, Dkt. Fikira S. Kimbokota, pamoja na viongozi waandamizi wa chuo.

Msafara huo ulianza ziara yake katika Kampasi ya Rukwa ya MUST, ambako walitembelea majengo mbalimbali yakiwemo madarasa mapya, karakana na maabara zinazotumiwa na wanafunzi kwa mafunzo ya nadharia na vitendo. Katika ziara hiyo, viongozi wa TCU walipata fursa ya kujionea kwa karibu maendeleo ya miundombinu na uwekezaji uliofanywa na chuo katika kuboresha mazingira ya ujifunzaji.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Profesa Kihampa alisema maendeleo yaliyofikiwa na chuo hicho ni makubwa ikilinganishwa na miaka ya nyuma alipowahi kupita katika Mkoa wa Rukwa. Alieleza kuwa hali ya sasa inaonesha mabadiliko chanya na uwekezaji wa makusudi katika elimu ya juu.

Aliongeza kuwa uongozi wa MUST unastahili pongezi kwa kusimamia kwa vitendo maelekezo na dira ya Serikali ya kuhakikisha vyuo vya elimu ya juu vinaweka miundombinu bora inayowawezesha wanafunzi kujifunza katika mazingira salama, rafiki na yenye tija.

Baada ya kukamilisha ziara katika Kampasi ya Rukwa, Profesa Kihampa aliendelea na ziara yake siku iliyofuata katika Kampasi Kuu ya MUST, ambako alitembelea maeneo mbalimbali ikiwemo madarasa, maabara na karakana zinazotumiwa na wanafunzi wa programu tofauti za sayansi na teknolojia. Katika kampasi hiyo, alionesha kuridhishwa kwake na ubora wa maabara, akibainisha kuwa zimejengwa na kuwekewa vifaa vya kisasa na adimu vinavyokidhi mahitaji ya mafunzo ya vitendo.

Profesa Kihampa alisema alishangazwa na kiwango cha uwekezaji kilichofanywa na chuo katika ununuzi wa vifaa vya maabara na miundombinu mingine ya kielimu, akieleza kuwa hatua hiyo ni kielelezo cha maono ya muda mrefu ya uongozi wa chuo katika kuinua ubora wa elimu ya juu.

kasi kubwa na kwamba ameridhishwa sana na maendeleo yaliyofanyika. AlimAk



Akizungumza na watumishi wa chuo, Profesa Kihampa alisema MUST imekua kwa kasi kubwa na kwamba ameridhishwa sana na maendeleo yaliyofanyika. Alimhakikishia Makamu Mkuu wa Chuo kuwa hoja ya awali ya ukosefu wa miundombinu sasa haina msingi, na akaahidi kuwa TCU haitasita kuidhinisha maombi ya chuo ya kuongeza idadi ya wanafunzi wa kudahiliwa pale yatakapowasilishwa, kutokana na uwezo wa miundombinu aliojionea.

Kwa upande wake, Makamu Mkuu wa Chuo, Profesa Aloys N. Mvuma, alimshukuru Profesa Kihampa kwa kutembelea MUST na kwa tathmini chanya ya maendeleo ya chuo. Alitumia fursa hiyo kuiomba TCU kutoa mrejesho kuhusu mitaala kadhaa ya programu za masomo iliyowasilishwa kwenye Tume hiyo, ili chuo kijue kama kinaweza kuanza kuitumia katika mwaka wa masomo wa 2025/2026 au kama kuna marekebisho yanayohitajika kabla ya kuanza utekelezaji.

Profesa Mvuma pia alimkaribisha Profesa Kihampa na uongozi wa TCU kuendelea kutembelea MUST mara kwa mara, akisisitiza kuwa ushirikiano kati ya Tume na vyuo ni muhimu katika kuhakikisha elimu ya juu nchini inakuwa na ubora, ushindani na mchango chanya katika maendeleo ya taifa.



13

# MUST kwa ushirikiano na UNIHUBS Yaweka Msingi wa Ujuzi wa Kidijitali

Mpango wa UNIHUBS unaendesha mafunzo ya ubunifu wa kidijitali na ujuzi wa ajira katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (Mbeya University of Science and Technology – MUST), ikiwa ni sehemu ya jitihada za kuimarisha uwezo wa taasisi za elimu ya juu katika kuandaa wahitimu wenye ujuzi unaokidhi mahitaji ya soko la ajira la sasa na la baadaye.

Mafunzo haya ni matokeo ya mradi wa pamoja baina ya MUST na Wroclaw University of Science and Technology (WUST), unaotekelezwa kupitia ufadhili wa Erasmus+ Programme. Mradi huo unalenga kuimarisha ubunifu wa kidijitali, ujuzi wa ajira na ushirikiano wa kitaaluma kati ya vyuo vikuu washirika wa kimataifa.

Mafunzo yanawahusisha wahadhiri na wanafunzi wa MUST, ambao wanapata fursa ya kujifunza kwa vitendo katika maeneo mbalimbali ikiwemo ufundishaji wa kidijitali, ujasiriamali, programu za kompyuta (coding), uchambuzi wa takwimu (data analytics), pamoja na namna ya kujenga ushirikiano imara na sekta ya viwanda na biashara.



*Dkt. Idelphonce Mkini akiwasilisha kuhusu uandaaji wa mtaala kwa wshiriki wa UNIHUBS*

Sehemu muhimu ya mafunzo inalenga masuala ya mtaala, ambapo washiriki wanasaidiwa kuchambua na kubuni upya kozi ili ziendane na mbinu za kisasa za ujifunzaji unaomweka mwanafunzi katikati, sambamba na kukuza ujuzi wa vitendo na wa kidijitali unaohitajika katika ulimwengu wa kazi.

Vipindi vya mafunzo vinaendeshwa kwa mtindo shirikishi na wa vitendo, vikihamasisha ubunifu, ubadilishanaji wa uzoefu na uundaji wa masomo shirikishi pamoja na suluhisho halisi kwa changamoto za kijamii, kiuchumi na kiteknolojia zinazowazunguka washiriki.



*Prof. Said A Vuai, akiwa kwenye picha ya pamoja na washiriki wa mradi wa **UNIHUBS***

Kwa ujumla, uzoefu huu unaendelea kuimarisha kujiamini kwa wahadhiri na wanafunzi, kuimarisha ushirikiano wa kimataifa kati ya MUST na washirika wake, pamoja na kuweka msingi imara wa kuwaandaa vijana wabunifu na wavumbuzi watakaokuwa na mchango mkubwa katika kuchagiza mustakabali wa kidijitali wa Tanzania.

# Makamu Mkuu wa Chuo Awahimiza Wanafunzi Wapya Nidhamu, Ubunifu na Uwajibikaji

Katika maadhimisho ya VC Day, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, Prof. Aloys N. Mvuma, amewahimiza wanafunzi wa mwaka wa kwanza kufuatilia ndoto zao za kielimu kwa nidhamu, bidii na dhamira thabiti, akisisitiza kuwa chuo kimejipanga kikamilifu kuwaunga mkono katika safari yao ya kitaaluma.

Profesa Mvuma amebainisha kuwa MUST inaendelea kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa kuhakikisha uwepo wa wahadhiri na watumishi wenye umahiri, pamoja na mitaala inayozingatia umahiri na ujuzi wa vitendo unaowaandaa wanafunzi kukabiliana na changamoto za ulimwengu wa kazi. Ameeleza kuwa dhamira ya chuo ni kuwaandaa wahitimu wanaojitegemea, wabunifu na wenye uwezo wa kutumia sayansi na teknolojia kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Akizungumza kuhusu wajibu wa wanafunzi, Makamu Mkuu wa Chuo aliwahimiza kutumia elimu wanayoipata kama nyenzo ya kutatua matatizo halisi ya jamii, sambamba na kuzingatia sheria, kanuni na maadili ya chuo. Alisisitiza kuwa mafanikio ya mwanafunzi hayapimwi tu kwa ufaulu wa kitaaluma bali pia kwa mwenendo, uwajibikaji na mchango wake kwa jamii.



*"Chuo hiki kimeweka mazingira wezeshi kwa wanafunzi kufanikiwa kupitia rasilimali watu wenye uwezo na mafunzo yanayolenga ujuzi, lakini mafanikio ya kweli yatategemea nidhamu, bidii na namna mtakavyotumia uhuru wenu kwa busara,"* ***alisema Profesa Mvuma.***

Aidha, Profesa Mvuma amewashauri wanafunzi wapya kutumia uhuru wao kwa umakini mkubwa, akiwatahadharisha dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya, matumizi yasiyokuwa na tija ya mitandao ya kijamii, pamoja na mienendo hatarishi inayoweza kuhatarisha afya na ustawi wao, ikiwemo maambukizi ya VVU/UKIMWI. Amehimiza wanafunzi kuzingatia masomo yao, kukuza vipaji, kushiriki shughuli za ubunifu na kujiendeleza kikamilifu katika nyanja zote za maisha ya chuo.





*Makamu wa Mkuu wa Chuo, Prof. Aloys Mvuma, akipokea zawadi kutoka kwa mwanafunzi wa mwaka wa kwanza*

Akihitimisha ujumbe huo, Rais wa MUSTSO amewahakikishia wanafunzi kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kinaendelea kutoa mazingira salama, rafiki kwa wanafunzi na yanayochochea ubunifu na ushirikiano. Amesema Serikali ya Wanafunzi itaendelea kushirikiana na uongozi wa chuo kuhakikisha wanafunzi wapya wanapata msaada na mwongozo unaohitajika wanapoanza safari yao mpya ya elimu ya juu.

# 15 WANAGENZI 310 WAHITIMU MAFUNZO YA KOZI MBALIMBALI CHUO KIKUU CHA SAYANSI NA TEKNOLOJIA MBEYA (MUST)

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) kimefanya mahafali ya 5 ya wahitimu wa kozi ya unagenzi, hafla iliyoratibiwa kwa ushirikiano na Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa hafla hiyo, Mkurugenzi wa Elimu Masafa na Endelevu, Dkt. Helikumi Mlyashimbi, alisema zaidi ya wanagenzi 3,000 waliomba nafasi za mafunzo hayo kupitia mpango wa serikali, ambapo MUST ilipokea wanafunzi 325 waliodahiliwa kusoma fani zaidi ya 10 ikiwemo ufundi umeme wa magari, ufundi jokofu, ufundi magari, ufundi bomba, na zingine nyingi.


Kiongozi wa wahitimu Bi Gift Fredy akipokea cheti cha uanagenzi kutoka kwa mgeni rasmi kaimu mkuu wa chuo Dkt buberwa Tibesigwa


Katika picha ni viongozi waliokuwa katika meza kuu siku ya mahafili ya wanagenzi kwa mwaka 2025


Katika picha ni wahitimu wa wanagenzi kwa mwaka 2025

**Dkt. Mlyashimbi** alisema kati ya hao, wanafunzi 310 wamehitimu rasmi mafunzo yao ya miezi sita, ambayo yalihusisha zaidi ya asilimia 70 ya mafunzo kwa vitendo, huku akieleza kuwa changamoto kadhaa zilijitokeza ikiwemo ucheleweshaji wa vifaa vya kujifunzia kutokana na taratibu za manunuzi na utoro wa baadhi ya wanagenzi.

Aidha, Dkt. Mlyashimbi aliipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuwekeza katika mafunzo ya vijana kupitia mpango wa wanagenzi, na kuiomba serikali kuongeza idadi ya wanagenzi wanaopelekwa MUST, akibainisha kuwa chuo sasa kina mazingira mazuri ya kufundishia na vifaa vya kisasa vinavyokidhi mahitaji ya mafunzo ya vitendo.

Kwa upande wake, mwakilishi wa wahitimu, Bi. Gift Fred, aliishukuru serikali inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fursa hiyo muhimu ya kujifunza ujuzi wa kazi. Alitoa wito kwa serikali kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wahitimu wa unagenzi, ili waweze kununua vifaa vya kazi watakavyovitumia kujiajiri na kutumia ujuzi walioupata MUST.

Mgeni rasmi wa mahafali hayo, ambaye pia ni Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo, Dkt. Buberwa Tibesigwa, aliwapongeza wahitimu wote na kuwataka kuwa mabalozi wazuri wa MUST kwa kuonyesha bidii, uadilifu na ubunifu katika kazi zao. Alisisitiza kuwa maadili na juhudi ndiyo nguzo kuu za mafanikio katika taaluma na maisha kwa ujumla.

Naye Kaimu Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia Fedha, Mipango na Utawala, Dkt Ramdhani Tekka alipokuwa akihitimisha hafla hiyo, aliwahimiza wahitimu kuwa kioo cha jamii, kufanya kazi kwa uaminifu na ubora, na kuepuka uvivu unaoweza kurudisha nyuma maendeleo yao binafsi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Elimu Masafa, Dkt. Malunguja, aliwahamasisha wahitimu hao kuunda vikundi vya kiuchumi na kuwasilisha katiba zao ili viweze kusajiliwa na kukopesheka kupitia mikopo ya Jiji la Mbeya, hatua itakayowawezesha kupata mtaji wa kuanzisha miradi ya kujiajiri na kuendeleza taaluma walizojifunza.

Mahafali hayo yaliambatana na burudani, hotuba za shukrani, na pongezi mbalimbali, yakionyesha mafanikio makubwa ya MUST katika kukuza ujuzi na kuongeza fursa za ajira kwa vi-



## Mawasiliano zaidi :

Fax : +255 (0) 25 2957552
Tel : +255 (0) 25 2957540/4 | +255 (0) 25 2957540/2
S.L.P 131 Mbeya - Tanzania
Email : vc@must.ac.tz